HOT &TOR – Kiswahili B

**T106**

Wednesday, 29/11/2017

02:00 – 05:00 PM

WORKFORCE DEVELOPMENT AUTHORITY

P.O. BOX 2707 Kigali, Rwanda Tel: (+250) 255113365

# Mtihani wa Taifa 2017

**SOMO: KISWAHILI B**

**MICHEPUO: HOTELI (HOT) NA UTALII (TOR)**

**MUDA: MASAA 3**

**MAELEZO:**

- Mtihani huu una sehemu tatu 1,2 na 3, una maswali 22 lakini utajibu maswali 18 tu kwa alama 100.
- Sehemu ya I ina maswali 14 ambapo unapaswa kuyajibu yote kwa alama 55.
- Sehemu ya II ina maswali 5 ambapo utajibu 3 tu kwa alama 30.
- Sehemu ya III ina maswali 3 ambapo utajibu swali moja tu kwa alama 15
- Andika vizuri nambari ya kila swali unalolijibu.
- Mwandiko wako usomeke na ujiepushe na uchafu.
- Tumia kalamu ya bluu au nyeusi .

## SEHEMU YA I: MASWALI 14 UNAPASWA KUYAJIBU YOTE KWA ALAMA 55

Ugonjwa hatari wa **ukimwi** umeenea kwa kasi sana katika nchi maskini ikiwemo nchi ya Rwanda.Kuna sababu mbalimbali zinazochangia hali hii. Sababu kubwa ni umaskini.

Wasichana na wanawake wengi hupenda kujiuza kama bidhaa sokoni ili wapate fedha ya kujikimu katika maisha yao. Hufanya hivyo kwa kujirahisisha kwa wanaume wenye **burungutu la fedha**. Wanawake hawa hujipeleka kwenye mabaa au kwenye vilabu vya pombe. Wakisha kunywa na **kuvaa miwani** wote huingia katika ulimwengu mwingine ambako huanza kuambukizana virusi vya ukimwi.

Sababu nyingine ni raha na starehe ambayo watu wengi hufurahia. Hufanya hivyo ili kujistarehesha wao wenyewe. Hutumia miili yao kama sehemu ya burudani katika maisha yao. Hukumbatiana ili kujisahaulisha taabu na **misukosuko** katika maisha.

Sababu nyingine ni ukosefu wa elimu juu ya ugonjwa huu. Watu wengi hawajafundishwa **athari** za ugonjwa huu kwa jamii. Hivyo hawajui maana ya ukimwi. Wao hufikiri kuwa ukimwi ni ndoto na hakuna ugonjwa wa aina hii! Hali hii imesababisha baadhi ya vijana kukataa kupimwa na kufanya mapenzi bila kutumia kondomu.

Njia zinazoeneza ugonjwa huu ni nyingi. Nikizitaja nitaonekana **mumbea** kwani kila mmoja anazifahamu. Athari za ukimwi katika jamii ni kama vile kifo, kushuka kwa shughuli za uzalishaji mali (ufanyaji biashara) n.k

**UFAHAMU NA MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 55**

**01.** Chagua jibu sahihi kati ya majibu yafuatayo:

Kichwa cha habari hii kinaweza kuwa: **/Alama 2**

- Ugonjwa hatari wa kisukari
- Ukimwi
- Ukosefu wa elimu
- Maisha rahisi ya wanawake

**02.** Zifuatazo ni njia zinazoeneza ugonjwa wa ukimwi, isipokuwa: **/Alama 2**

- Kupenda pesa kwa wasichana na kufanya ngono
- Elimu chache juu ya ugonjwa huo
- Kufanya mapenzi bila kutumia kondomu
- Jamii hufa sana kwa sababu ya ukimwi

**03.** Katika habari hii neno "**burungutu**" humaanisha: **/Alama 2**

- Pesa za kusaidia maskini
- Pesa nyingi mno
- Pesa chache sana
- Fedha walizoiba

**04.** Sababu kubwa ya ueneaji wa ukimwi iliyotajwa ni: **/Alama 2**

- Ufukara
- Mafarakano
- Kuvaa miwani
- Bulungutu la fedha

**05.** …… wote huingia katika ulimwengu mwingine ambako …. Neno **ulimwengu mwingine** walitarajia kumaanisha: **/Alama 2**

- Dunia nyingine
- Taifa ya mbali
- Kupoteza fahamu
- Kutotumia kondomu

**06.** Taja sababu tano zinazochangia katika ueneaji wa ugonjwa wa ukimwi katika nchi maskini kama Rwanda. **/Alama 5**

**07.** Toa angalau njia tano za kujilinda ugonjwa wa ukimwi. **/Alama 5**

**08.** Je, unakubaliana na mwandishi huu kuwa sababu kubwa ya ueneaji wa ukimwi ni umaskini? Kwa nini? **/Alama 4**

**09.** Onyesha namna vijana wengi hutumia miili yao kama sehemu ya burudani. **/Alama 3**

**10.** Katika maelezo yako fasaha, eleza misamiati ifuatayo kutoka kifungu cha habari hapo juu. **/Alama 10**

- ✰ UKIMWI
- ✰ Misukosuko
- ✰ Kuvaa miwani
- ✰ Athari
- ✰ Mumbea

**11. Tegua vitendawili vifuatavyo.** **/Alama 4**

- Tunamsikia lakini hatumwoni ...........
- Ni mfalme lakini hana raia wala askari .........
- Juu mboga, kati kuni, chini chakula ..........
- Watoto wangu wote nimewavika kofia nyekundu ..........

**12. Eleza nahau na misemo vifuatavyo.** **/Alama 5**

- ❖ Kufa kupona
- ❖ Mkono wa birika
- ❖ kuwa mtungi
- ❖ Pua na mdomo
- ❖ Mbuzi

**13. Jaza methali zifuatazo.** **/Alama 5**

- ➢ ............... Hujenga ukuta
- ➢ bandu bandu ............
- ➢ .................. Huvunjika guu
- ➢ Adhabu ya kaburi ..........
- ➢ ........ usifikiri ni utajiri

**14. Tofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi.** **/Alama 4**

## SEHEMU YA II: MASWALI 5 AMBAPO UTAJIBU 3 TU KWA ALAMA 30

**SARUFI** **(Jibu maswali matatu tu)**

**15. Kanusha ama uyakinishe sentensi zifuatazo.** **/Alama 10**

- **a.** Amkeni!
- **b.** Kijana huu hategemei msada wa wazazi wake kwa kulipa karo za shule.
- **c.** Kula nyama nyekundu husaidia watoto kukuwa vizuri.
- **d.** Fisi hupenda kujificha porini.
- **e.** Lililo lako usililie.

**16.** Unda sentensi tano ukitumia jedwali lifuatalo na aina za maneno zilizomo. **/Alama 10**

| Kitenzi | Nomino | kivumishi | Kiunganishi | nomino | Kivumishi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kuliko | | |
| | | | Pamoja na | | |
| | | | na | | |
| | | | kwa | | |

**17. Tunga sentensi tano ukitumia maneno yafuatayo (sentensi moja kwa kila neno):**

*Jana, kila mara, kesho kutwa, leo, dakika chache zilizopita.* **/Alama 10**

**18. a.** Taja aina za tungo uzijuazo ukizingatia msingi wa muundo? **/Alama 4**

**b.** Kwa uchaguzi wako chagua aina tatu kati ya hizo ulizozitaja hapo juu kisha utunge mfano mmoja mmoja kwa kila aina. **/Alama 6**

**19.** **Jaza nafasi wazi katika tungo zifuatazo ukitumia neno maalumu kutoka kwa maneno yafuatayo:** *la, ya, zipi, mingine, yake, ipi, wote, wenyewe, wepi, kupi* **/Alama 10**

- ☆ Hoteli .... umeiaminia nchini humu?
- ☆ Daftari .... Kiswahili.
- ☆ Walimu .... wanakufundisha lugha ya Kiswahili?
- ☆ Maziwa ...... mtoto
- ☆ Sisi ...... tutaijenga taifa yetu.
- ☆ Nyanya ...... anagonjwa.
- ☆ Kuta ...... zina nyufa nyingi?
- ☆ Shemeji ......... walimtembelea siku moja baada ya kuzaliwa mtoto wa nne.
- ☆ Mahali ...... ni kuzuri kwa watalii kutembelea?
- ☆ Miti .... inazaa matunda kwa wingi?

**SEHEMU YA III: MASWALI 3 AMBAPO UTAJIBU SWALI MOJA TU KWA ALAMA 15**

---

**UTUNGAJI** **(chagua swali moja la kujibu)**

**20.** Mradi wa serikari wa maendeleo 2020 (Vision 2020), utafaulu lengo lake. Pinga au utetee kauli hii kati ya mistari kumi na kumi na mitano. **/Alama 15**

**21.** Kwa kuvutia watalii kutoka nje ya Rwanda, tunga insha kati ya mistari kumi na kumi na mitano ukiwaonyesha sehemu za kuvutia za Rwanda. **/Alama 15**

**22.** Kama mwanafunzi na kijana anayetegemewa kuiongoza Rwanda ya kesho, Tunga insha kati ya mistari kumi na kumi na mitano ukitowa mifano na kueleza umuhimu wa wanyama wafugwao na wale wasiofugwa. **/Alama 15**

Blank page